20:1-31:13 SAULI AMWUDHI DAUDI

Yonathani amsaidia Daudi kutoroka (20:1-42)

Inaonekana kama Yonathani hakujua kwamba baba yake alijaribu kumwua Daudi mara kwa mara (20:1-2). Alipoona kwamba Daudi alikuwa na hofu kubwa, alikubali kusaidiana naye, ili ajue kabisa madhumuni ya Sauli kuhusu maisha ya Daudi (3-9).

Yonathani alisimama imara kabisa katika upendo wake kwa rafiki yake. Ingawa alijua wazi kwamba Daudi angekuwa mfalme badala ya Sauli, wala si yeye, hakuonyesha dalili yo yote ya wivu. Ila jambo moja alimwomba Daudi, yaani kama angekuwa mfalme, aendelee kuwa mwaminifu kwa Yonathani, na aonyeshe uaminifu huo kwa wazao wake pia (10-15). Wote wawili waliapa kuwa waaminifu kila mmoja kwa mweziwe, na hivyo walithibitisha agano lao (16-17).

Daudi na Yonathani walijadiliana maarifa ya kuona kama ingefaa Daudi aendelee kudumu katika utumishi wa Sauli, au atoroke kwa ajili ya usalama wake. Makusudi yao yalikuwa kuokoa maisha ya Daudi. Hawakufanya njama dhidi ya mfalme, na walipotunza sana siri yao, walihakikisha kwamba maneno yao yasingeweza kuenezwa kwa namna ya porojo (18-23).

Hata Sauli alipojaribu kumwonyesha Yonathani kwamba Daudi angekuwa hatari kwa maendeleo na maisha yake, Yonathani aliendelea kuwa mwaminifu kwa Daudi bila ubinafsi wo wote (24-31). Sauli akamlaumu Yonathani kuwa hata yeye si mwaminifu kwa ukoo wake, akajaribu kumwua (32-34). Wakati huo Yonathani hakuwa na mashaka yo yote tena juu ya madhumuni ya baba yake. Kwa huzuni kubwa yeye na Daudi waliagana, Daudi akaondoka (35-42).

Daudi amtoroka Sauli (21:1-15)

Sehemu ya kwanza Daudi alipokimbilia ilikuwa mji wa Nobu ambao, baada ya kubomolewa kwa Shilo, ulikuwa mji wa makuhani (21:1). Wakati huo watumishi wachache wa binafsi walijiunga na Daudi, kufuatana na mapatano fulani yaliyofanywa awali kidogo. Daudi alipokea chakula kwa ajili yake na watu wake kwa njia ya kumdanganya kuhani Ahimeleki kuhusu makusudi ya safari yake. Kwa bahati mbaya, kwa yeye mwenyewe, kwa Ahimeleki na makuhani wengine, Daudi alionekana na mtu aliyekuwa rafiki wa Sauli (2-9).

Kutoka Nobu, Daudi alikwenda Gathi, mji wa Wafilisti. Alifikiri kwamba Wafilisti wangemkaribisha, yeye akiwa mtoro wa jeshi la Israeli, na kumpa nafasi ya kujificha (10). Lakini Wafilisti walikuwa hawajasikia habari za kutengana kwake na Sauli. Walichojua na kukumbuka ilikuwa kwamba Daudi aliua Wafilisti wengi. Walifikiri safari hiyo ilikuwa ya kupeleleza hali ya nchi na kuandaa mashambulio mapya wakaamua kumwua. Daudi alipaswa kujifanya kana kwamba ni mwenda wazimu, kusudi aweze kuokoa maisha yake na kutoroka (11-15; taz.Zab 34 na 56).

Daudi aunda jeshi lake mwenyewe (22:1-23)

Daudi alipata maficho katika maeneo ya jangwa na ukiwa wa Adulamu. Huko alikutana na watu wa familia yake waliokuwa wamekimbia hasira na kisasi cha Sauli, (22:l;taz. Zab 57, 63 na 142). Hali akijua kwamba maisha yake magumu yasingefaa kwa wazazi wake waliozeeka, aliwaacha katika utunzaji wa mfalme wa Moabu, kisha yeye akarudi katika nchi yake ya Yuda. Wakati huo kundi kubwa la watu kama 400 hivi walishirikiana naye, ambao wengi wao walikuwa watu wenye dhiki, madeni au uchungu fulani, wasioweza kuishi maisha ya kawaida. Watu hao Daudi aliwaunganisha kuwa jeshi lenye nguvu (2-5; lNya 11:10,15).

Miongoni mwa watu wale waliojiunga na Daudi walikuwepo askari wengi wenye uzoefu wa vita ambao walikuwa wametoroka kutoka makabila ya mashariki, pamoja na wengine wa Wabenyamini na Wayuda. Siku zote Daudi aliangalia sana kuhakikisha kwamba hakuwakaribisha wapelelezi au watu wengine waliotumwa na Sauli ili kumwangamiza (lNya 12:8-18). Baada ya muda alikuwa na jeshi la watu 600 (taz.23:13). Wakati wote wa kuudhiwa na Sauli, Daudi na watu wake walikuwa katika eneo la kabila lake Daudi, yaani la Yuda. Lakini mara nyingine walifukuzwa kwenda kusini zaidi katika maeneo ya ukame na jua kali, au magharibi katika maeneo yaliyotawaliwa na Wafilisti.

Wakati huo Sauli aliwalaumu watumishi wake kwamba wao si waaminifu kwake na kumsaidia Daudi. Sauli aliwakumbusha kwamba angewapa misaada na zawadi mbalimbali, kwa sababu walikuwa wa kabila lake la Benyamini. Wasingepata kitu cho chote kwa Daudi, kwa sababu yeye angewapendelea watu wa kabila lake tu (6-8).

Sauli alipogundua kwamba Ahimeleki alikuwa amemsaidia Daudi, Ahimeleki alijitetea akisema kwamba, ilikuwa kwa uaminifu wake kwa Sauli tu kwamba alimsaidia Daudi. Yeye akifikiri Daudi alikuwa ametumwa kuzitimiza shughuli za Sauli tu (9-15). Wakati huo Sauli alikuwa na hasira kiasi kwamba asiweze kusikia neno la maana, akaamuru si kumwua Ahimeleki tu, bali na makuhani wote wa Nobu pia. Abiathari peke yake aliweza kutoroka, naye mara moja alimwendea Daudi na kujiunga naye (16-23; taz.Zab 52)

Uwindaji wa hasira wa Sauli (23:1-24:22)

Baada ya Abiathari kuchukua pamoja naye naivera ya kuhani mkuu (pamoja na Urimu na Thumimu), Daudi aliweza kuuliza na kupata jibu moja kwa moja kuhusu uongozi wa Mungu. Agizo la kwanza la Mungu lilikuwa kuuokoa mji wa Israeli wa Keila kutoka kwa Wafilisti waliokuwa wakiiba nafaka huko (23:1-6). Mara baada ya kuwapiga Wafilisti, Daudi aliondoka Keila, akijua kwamba jeshi la Sauli lilikuwa kubwa na lenye silaha nyingi zaidi kuliko lake. Pi a watu wa Keila hawakuaminika kama wangejiunga na Daudi na kumzuia Sauli. Daudi alikuwa bado anamtambua Sauli kuwa mfalme wa halali. Hakuwa na haja yo yote ya kushindana naye, wala kuwashawishi watumishi wa Sauli wamfitini mfalme wao (7-13).

Daudi alijificha katika misitu ya nchi ya milima karibu na Zifu, na Yonathani alikuja kumtembelea. Yonathani aliendelea kuwa mwaminifu kwa Sauli kama mfalme wa halali, lakini alimhakikishia Daudi upya kwamba, hakuna jambo lo lote ambalo lingeweza kuharibu uhusiano uliokuwepo baina yao (14-18).

Sauli alifurahi, lakini Daudi alisikitika, baadhi ya watu wa Zifu walipomwambia Sauli maficho ya Daudi (23:19-24; taz.Zab 54). Daudi alinusurika hatari ya kukamatwa, Sauli alipopaswa kurudi kwa haraka na kuwazuia Wafilisti walioshambulia na kuiba katika Israeli (25-29).

Baada ya kushughulika na Wafilisti, Sauli aliendelea na adha yake dhidi ya Daudi. Inaonekana kama katika watu wa Sauli walikuwepo wengine wenye bidii sana ya kumsaidia Sauli, labda Wabenyamini, ambao walimshtaki Daudi kwamba yeye alitaka kumpindua mfalme, nao wakamhimiza Sauli kumwangamiza Daudi (taz. 18:22-26; 22:7; 24:9; 26:19; Zab 7). Kwa njia ya kuyaokoa maisha ya Sauli ambapo angaliweza kumwua kwa urahisi, Daudi alionyesha haki yake na usafi wa roho yake ambao siku zote ni alama ya mfalme wa kweli (24:1-15). Hata Sauli alikubali hayo. Ilikuwa kama tendo la Daudi la kuokoa maisha ya Sauli halijatosha, Sauli alimwomba Daudi kutoa ahadi kwamba, baada ya kuwa mfalme asiwaue watu wa ukoo wake. Lakini Sauli hakuahidi kumwokoa Daudi. Kwa hiyo Sauli aliporudi nyumbani, Daudi aliona ingekuwa salama zaidi kurudi katika maficho yake (16-22).

Daudi amwoa Abigaili (25:1-44)

Sehemu hii tunaambiwa kwamba Samweli alikufa (25:1). Wakati huo Daudi alikuwa na shida ya kupata chakula kwa watu wake 600. Inaonekana kama watu wake waliwasaidia wakulima kulinda mashamba yao dhidi ya Wafilisti waliotaka kuiba nafaka yao (taz.mist. 16,21), kisha wakawadai wenye mashamba kuwalipa kwa njia ya kuwapa chakula (taz.mist.8,18,27,35). Tajiri mmoja, Nabali, alikataa kulipa akamtukana Daudi. Daudi akiwa amekasirika juu ya mambo ya Nabali, aliondoka na watu 400 wa watu wake ili kumwadhibu (2-13).

Ilikuwa kwa sababu ya maarifa ya haraka na maneno ya hekima ya mke wa Nabali, Abigaili tu, kwamba Daudi hakumwangamiza Nabali na nyumba yake. Abigaili alimpelekea Daudi chakula kilichodaiwa (14-22), akamwonya aendelee na kumtegemea Mungu ili amlinde na kuwaangamiza maadui zake. Bila shaka Daudi asingefanya jambo lo lote ambalo baadaye angelijutia (23-31).

Daudi alishukuru kwa chakula na kwa ushauri wa Abigaili. Baada ya muda mfupi tu matukio yalithibitisha maneno ya Abigaili. Mungu alimwondoa adui wa Daudi, Nabali alipopata ugonjwa wa ghafla na kufariki (32-38). Kisha Daudi akamwoa Abigaili, na kwa njia hii akawa mshiriki wa mwenye eneo kubwa la mashamba mazuri katika nchi ya Yuda (39-42). Lakini alipotewa na mkewe Mikali, Sauli alipomchukua binti yake na kumpa mtu mwingine (43-44).

Daudi ahamia nchi ya Wafilisti (26:1-27:12)

Ingawa Daudi alikuwa akitaka kumwua Nabali, alikataa kabisa kumdhuru Sauli, ingawa Sauli alitaka kumdhuru Daudi daima (26:1-5). Angaliweza kumwua Sauli kwa urahisi tena, lakini aliridhika kumtegemea Mungu kwamba Yeye angemwondoa adui yake katika wakati wake (6-12).

Daudi alikuwa amethibitisha tena kwamba hakutaka kumdhuru Sauli (13-17). Lakini hata hivyo alichoka kumtoroka Sauli mara kwa mara, si kwa sababu mambo hayo yalimchosha tu, bali kwa sababu yalimtenga na Mungu, yaani alishindwa kwenda sehemu maalumu za ibada ya taifa lake Israeli (18-20). Sauli alikiri makosa yake na kuahidi kwamba asingemdhuru Daudi, lakini Daudi bado alifikiri ingekuwa bora kuishi mbali naye sehemu za kusini kabisa (21-25).

Mambo yalikuwa mabaya zaidi Daudi alipoondoka katika nchi yake na kutafuta usalama katika nchi ya maadui Wafilisti. Wakati huo Akishi, mfalme wa Wafilisti, alimkaribisha, kwa sababu alijua kwamba Daudi alikuwa adui wa Sauli, wala si mmojawao wa maakida wake (kwa habari ya safari ya kwanza ya kukutana na Akishi, taz.21:10-15). Pia jeshi la Daudi, ambalo kwa wakati huo liliimarika kwa sababu ya askari wake Wabenyamini wenye uzoefu mwingi wa vita (lNya 12:1-7), lingeweza kuwafaa Wafilisti. Daudi kwa hekima yake, aliomba na kupata mji wa peke yake, yaani Siklagi, ili aishi huko pamoja na watu wake, na hivyo aliweza kuzuia matata na Wafilisti, pia kuwa na watu wake mahali pamoja wakiwa jeshi lake la kutegemewa. Aliishi huko Siklagi kwa muda wa miezi 16 (27:1-7).

Wakati ule hauonekani kuwa ulimsaidia Daudi sana kiroho. Mambo yaliyompata hapo awali alipomkimbia Sauli sehemu mbalimbali katika nyika za Yuda, yalimjenga kiroho, na wakati ule alitunga Zaburi nyingi. Kinyume chake wakati wa kukaa kwake kwa Wafilisti, ulikuwa na mambo mengi ya aibu, wala hatuna habari ya Zaburi yo yote iliyoandikwa wakati huo.

Daudi alimpendeza Akishi na kuwatajirisha Wafilisti kwa njia ya mashambulio mbalimbali ambayo Akishi alifikiri kwamba yalikuwa dhidi ya Waisraeli au makabila ya urafiki wa Waisraeli. Lakini kwa kweli yalikuwa dhidi ya watu wengine wa jangwani, ambao kwa kawaida walikuwa maadui wa Waisraeli. Kwa aibu yake, Daudi aliwaagiza watu wake kuwaua wenyeji wote wa miji aliyoishambulia. Kwa njia hii alihakikisha kwamba hawakubaki watu walioweza kumwambia Akishi habari za kweli kuhusu watu ambao Daudi aliwashambulia (8-12).

Vita vingine vya Wafilisti na Waisraeli (28:1-29:11)

Wafilisti walipojiandaa kuwashambulia Waisraeli tena, Akishi alimfanya Daudi na watu wake kuwa walinzi wake binafsi (28:1-2). Huko Israeli Sauli alihangaika sana. Alikuwa amemwuliza Mungu la kufanya, lakini Mungu hakumjibu (3-6). Hivyo alimwendea mwanamke aliyeweza kuwaitisha mahoka (yaani mizimu au roho za watu waliokufa), akitumaini kwamba kwa njia hiyo angeweza kupata uongozi wa Samweli (7-14).

Samweli alirudia maneno yale yale tu ambayo alikwisha mwambia hapo awali kwamba Mungu alimkataa. Alimweleza kwamba Daudi alikuwa mtu ambaye Mungu alimchagua kuwa mfalme badala yake, akaongeza kusema kwamba, yeye Sauli pamoja na wanawe wangekufa katika vita vilivyowakabili (15-19). Hapo Sauli alitishwa zaidi kuliko wakati wote, lakini mwanamke yule alimpa chakula ili kumtia nguvu kwa ajili ya mashambulio yaliyomkabili (20-25).

Viongozi wa Wafilisti pia walikuwa na matatizo yao. Watawala wanne walioshiriki utawala pamoja na Akishi walikuwa na mashaka walipomwona Daudi pamoja na watu wake 600 miongoni mwa majeshi yao. Walikumbuka ushindi wa zamani wa Daudi dhidi ya Wafilisti, nao waliogopa kwamba, huenda katikati ya vita Daudi na watu wake wangegeuka na kuwasaidia Waisraeli (29:1-5). Kwa hiyo waliwarudisha Daudi na watu wake waende Siklagi. Daudi alisikitika juu ya uamuzi huo, kwa sababu inawezekana kwamba aliazimu kufanya vile ambavyo Wafilisti walikuwa na wasiwasi naye. Kwa upande mwingine, inawezekana kwamba viongozi wa Wafilisti kwa njia hii walimzuia Daudi asifanye ujinga, kwa sababu kama angalikuwa amewashambulia watu wake mwenyewe katika vita, ingalikuwa vigumu baadaye kwa watu hao kumkubali kuwa mfalme wao (6-11).

Ushindi wa Daudi na kuanguka kwa Sauli (30:1-31:13)

Watu wa Daudi waliporudi Siklagi, walikuta kila kitu kimeharibika na nyumba zote zimechomwa moto. Waamaleki walikuwa wameshambulia miji ya Wafilisti na ya Yuda, wakati askari wao walipokuwa wangali vitani. Akishtushwa sana na habari ya kupotelewa na kila kitu, yaani wake zake, watoto na mali yote, Daudi alibakiwa na jambo moja tu, yaani kumtegemea Mungu wake. Aina hii ya kumtegemea Mungu kabisa inaonekana kama ilikuwa imempotea Daudi kwa muda ule wote wa miezi 16 aliyokuwa akikaa katika nchi ya Wafilisti (30:1-8).

Akisaidiwa na maakida wengine wa Israeli ambao kabla ya muda mfupi walitoroka katika jeshi la Israeli na kujiunga naye (lNya 12:19-22), Daudi aliondoka kuwafuatia Waamaleki. Alisaidiwa pia na

mtumwa wa Waamaleki aliyeachwa njiani ili afe; lakini baada ya kusaidiwa aliweza kumwonyesha Daudi kambi ya Waamaleki (9-15). Watu wa Daudi waliwaua Waamaleki wakarudisha watu na vitu vyote vilivyoibwa, kisha wakateka nyara mali nyingi sana kutoka kwa Waamaleki (16-20).

Alipogawanya mateka miongoni mwa watu wake, Daudi alitoa mafungu sawa kwa wale walioshambulia na wale waliobaki kambini na matendo ya ukatili na ya aibu ambayo kulinda vitu vyao (21-25). Pia aligawanya sehemu ya angetendewa na maadui kama wangemkamata, na mateka katika miji ya Yuda na katika makabila hivyo alijiua mwenyewe (31:1-7). Kwa hiyo madogo ya karibu, na hivyo aliwapa watu wale maadui walifanya michezo ya aibu na maiti yake. sababunzuri ya kujiunga naye baadaye (26-31). Lakini watu wa Yabeshi-gileadi walikumbuka Wakati huo huo sehemu za kaskazini vita vya matendo makubwa ambayo Sauli aliwafanyia Waisraeli na Wafilisti viliendelea kwa nguvu sana. awali katika kuwaokoa kutoka kwa maadui zao,Baada ya kushindwa na maadui zao, Waisraeli kwa hiyo walichukua maiti yake na kumfanyia walikimbia. Wana wa Sauli waliuawa, na Sauli mazishi ya heshima (8-13: taz.l 1:1-11; lNya mwenyewe alijeruhiwa vibaya. Sauli alijua 10:13-14).